JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

31 MEI, 2016

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU – 31 MEI, 2016

I. KIAPO CHA UAMINIFU:

1. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

266. MHESHIMIWA SUSAN ANSELIM LYIMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Elimu bora ni uti wa mgongo wa maendeleo ya jamii yoyote ile na msingi bora wa elimu kwa watoto unaanzia toka shule za awali na za msingi:-

(a) Je, kuna shule ngapi za awali kati ya mahitaji halisi;

(b) Je, ni nini mipango ya haraka kuhakikisha shule za awali zinakuwepo katika shule zote za msingi za Serikali nchini.

267. MHESHIMIWA RASHID MOHAMED CHUACHUA (MASASI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Masasi lina shule moja tu ya Sekondari kwa kiwango cha Kidato cha tano na sita ambayo ni Sekondari ya Wasichana Masasi ambayo imekuwa haitoshelezi kutokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaofaulu:-

(a) Je, ni lini Serikali itazipandisha hadhi shule za Sekondari za Mwenge Mtapika na Anna Abdalla ili ziweze kupokea wanafunzi wa Kidato cha tano na sita;

(b) Je, ni lini Serikali itaajiri Walimu katika Jimbo la Masasi ikiwa Ikama ya Walimu wa Sayansi katika shule za Sekondari 9 zilizopo ni walimu 84 lakini waliopo ni 24 tu.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

268. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mkoa wa Kigoma umekumbwa na wimbi kubwa la Wakimbizi wa kutoka Burundi na Congo DRC na kutokana na wimbi hilo ujambazi umeongezeka sana:-

Je, Serikali iko tayari kuongeza Ulinzi na vitendea kazi vya kutosha ili Mamlaka husika iweze kukabiliana na tatizo.

269. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Mgodi wa GGM - Geita unaongoza kwa kuwapiga vijana risasi na kuwachapa viboko na pengine kuwasababishia vifo lakini wahusika hawachukuliwi hatua stahiki:-

Je, Serikali inachukua hatua gani sasa dhidi ya wahusika pale inapotokea wameua watu au kujeruhi.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

270. MHESHIMIWA ALMASI ATHUMANI MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- sehemu kubwa ya Jimbo la Tabora Kaskazini, Uyui haina maji chini ya ardhi na hivyo wananchi hawawezi kupata maji kwa kuchimba visima. Wananchi wanaipongeza Serikali kwa kubuni mradi wa kuleta maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria kupitia Shinyanga, Kahama, Nzega mpaka Isikizya na maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo ili wananchi wa Jimbo la Tabora Kaskazini katika Vijiji vya Isikizya, Upuge, Majengo na Kanyenye wapate huduma ya maji;

(b) Kwa kuwa bomba hilo la maji litatoa maji kwa umbali wa km. 25 kuwafikia wananchi wachache. Je, Serikali haioni kuna sababu ya kuanzisha mradi wa kuchimba mabwawa na kukinga maji ya mvua kama chanzo kingine cha maji kwa wananchi.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

271. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Hapo zamani kulikuwa na Shirika la Uvuvi la TAFILO lenye makao makuu yake Kigamboni ambalo lilikufa kutokana na uendeshaji mbovu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Shirika hilo;

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kusimamia *"deep fishing"* ili iweze kunufaika na mapato yatokanayo na uvuvi.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

272. MHESHIMIWA UPENDO FURAHA PENEZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Kufuatia vifo vyenye utata vya kisiasa na vinavyohusisha vyombo vya dola, aliyekuwa Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda alitoa ahadi katika Bunge la Kumi ya Serikali kuunda Mahakama ya *Coroner* (*Coroner's court*) kwa ajili ya kuchunguza vifo mbalimbali vyenye utata:-

Je, Serikali iko katika hatua gani kutekeleza ahadi hiyo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

273. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIA BUKWIMBA (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga barabara ya Geita – Bukoli – Kahama kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hiyo.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

274. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina uhakika gani na usalama wa nchi yetu katika mpaka wa Pori la Akiba la Kimisi na Buligi na mto Kagera.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

DODOMA
31 MEI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE